# Learning by Ear – Climate Change

**Episode 10**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

Scene 1:

- MRS CHRISTINE KIMASI – RENEWABLE ENERGY INVESTOR (50)
- CAROL (14)
- LORNA (16)
- ALEX (15)
- JOSHUA (15)

Scene 2:

- LORNA (16)
- MRS KIMAU – LORNA'S MOTHER (45)
- RADIO PRESENTER

Scene 3:

- ALEX (15)

- JOSHUA (15)
- LORNA (16)
- CAROL (14)
- MR KAPOOR – NATIONAL POWER BOARD (60)
- MRS KIMASI – RENEWABLE ENERGY INVESTOR (50)
- JOURNALIST 1 (FEMALE 25)
- JOURNALIST 2 (MALE 30)

**Intro:**

Karibu msikilizaji katika kipindi hiki cha mwisho cha mchezo wa redio kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa. Jopo maalum limefanya kila linaloweza kuwashawishi wanachama wa bodi ya umeme ya kitaifa, kubadili mipango yao na kuupa mji wa Dhowville nishati inayoweza kutumiwa tena na isiyochafua mazingira. Je jopo hilo litafanikiwa kutimiza jukumu lake katika kupunguza mabadiliko ya hali ya hewa? Tega sikio ufahamu nini kitakachotokea mwishoni mwa hadithi hii.

**Scene One: Restaurant**

| | |
|---|---|
| **SFX ATMO:** | **DINERS/CUTLERY/MUSIC** |
| **1. MRS KIMASI:** | Ee mkutano huo umekuwa mkutano wa kipekee kabisa! |
| **2. JOSHUA:** | Umenena! Nilidhani bwana Kapoor alikaribia kugeuka na kutoka nje ya mkutano alipotuona tumekaa pale. |
| **3. CAROL:** | Mimi pia nilifikiri hivyo, Joshua! |
| **4. MRS KIMASI:** | Labda angetoka mkutanoni kama waziri wa mazingira hangekuwa upande wetu kutuunga mkono. Sawa tuagize chakula. Mimi leo nitagharamia chakula hiki cha mchana. |
| **5. CAROL:** | Nahisi njaa sana! |

**6. LORNA:** Lakini Bi Kimasi nini hasa kilichokuvutia katika sekta ya nishati hii inayoweza kutumika tena na tena?

**7. MRS KIMASI:** Niliishi na kufanya kazi nchini Nigeria, magharibi mwa Africa kwa miaka minane, na niliyoshuhudia huko katika sekta ya mafuta yalinifanya kuapa kufanya kila nitakaloweza kuona bara la Afrika linafuata mkondo wa nishati inayoweza kutumika tena na tena na kukomesha mabadiliko ya hali ya hewa.

**8. JOSHUA:** Nini kinachoendelea nchini Nigeria ambacho kinaudhi?

**9. MRS KIMASI:** Kama unavyojua Nigeria ni taifa linalotoa mafuta kwa wingi. Kimsingi sekta ya mafuta ndio ndiyo nguzo ya uchumi wote nchini humo.

**10. CAROL:** Ingawa bado ni taifa maskini sana?

**11. MRS KIMASI:** Ndio – Lakini kabla ya kuuza mafuta yake kwa nchi nyingine, Nigeria hutumia mfumo wa kusafisha mafuta kwa kuchoma sehemu ya gesi iliyochanganyika na mafuta hayo. Mafuta ya petroli yanapochimbwa huwa yamechanganyika na gesi. Nchini Nigeria gesi hii huchomwa ili kuhakikisha mafuta ya kiwango cha juu cha ubora yanabakia.

**12. JOSHUA:** Na kuna ubaya gani kuichoma gesi hiyo?

**13. MRS KIMASI:** Aaah tafiti kadhaa zinadai kwamba kiasi cha robo ya gesi inayochafua mazingira barani Africa htokana na uchomaji wa gesi ya mafuta nchini Nigeria.

**14. ALEX:** Robo!- hicho ni kiwango kikubwa sana!

**15. MRS KIMASI:** Pia ni uharibifu mkubwa sana. Ungeweza kutoa umeme kwa nchi nyingi barani Afrika kutumia gesi hiyo inayochmwa nchini Nigeria. Katika mataifa mengine, gesi hii hutumiwa na kuuzwa au angalau kurejeshwa ardhini. Lakini kuichoma kama wanavyofanya nchini Nigeria ni uharibifu mkubwa wa nishati!

**16. LORNA:** Nafikiri kuchoma kiwango kikubwa namna hiyo cha gesi pia kunaathiri mazingira ya eneo hilo..

**17. MRS KIMASI:** Ndio. Jamii zinazoishi karibu na eneo hilo huhangaika sana kupata maji safi ya kunywa hulalamika kuhusu uchafuzi wa hewa. Ni janga kubwa kwa mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira.

| | |
|---|---|
| **18. CAROL:** | Kwa hivyo, hiyo ndio sababu ukajiingiza katika sekta hii ya nishati inayoweza kutumiwa upya? |
| **19. MRS KIMASI**: | Ndio, nishati asili kama vile mafuta, makaa ya mawe na gesi asili, zitaisha wakati fulani. Na nishati asili huongeza kiwango cha ujoto na kutoa gesi chafu wakati zinapochomwa. Tunahitaji kuangalia nishati mbadala inayoweza kutumika tena na tena na isiyochafua mazingira. Huo ndio mustakabali wetu! |
| **20. LORNA:** | Chakula chetu kimefika - nani ameagiza sandwichi ya kuku? |
| **21. CAROL:** | Mimi hapa! |
| **22. MRS KIMASI:** | Sawa tuleni basi! Bado tuna kazi kubwa ya kufanya alasiri ya leo. Natarajia kupigiwa simu na bodi ya taifa ya umeme kutujulisha uamuzi wao waliofikia! |

| | |
|---|---|
| **SFX:** | **CUTLERY/EATING** |

**Scene Two: Lorna’s House**

| | |
|---|---|
| **SFX ATMO:** | **SEWING MACHINE** |
| **23. LORNA:** | Shikamoo Mama, uko nyumbani? |
| **24. MRS KIMAU:** | Ndio niko chumba cha nyuma huku.. |
| **SFX:** | **RADIO NEWS TUNE** |
| **25. LORNA:** | Ah, Shikamoo Mama? Unashona? |
| **26. MRS KIMAU:** | Marahaba Lorna, ndio, shhhhh …. Hebu subiri kidogo! |
| **27. PRESENTER:** | Ziara ya leo ya mwakilishi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, inafanyika wakati ambapo taifa linakumbwa na uhaba mkubwa wa mahindi na nafaka nyingine. Wataalam wanayanyoshea kidole mabadiliko ya hali ya hewa na kuihimiza serikali na wafadhili kuchukua hatua za haraka kukabilianana kitisho hiki kwa uhakika wa upatikanaji wa chakula. |

| | |
|---|---|
| **28. LORNA:** | Kwani chakula kinakaribia kuisha mama? |
| **29. MRS KIMAU:** | Bado, lakini kama ulivyosikia mabadiliko ya hali ya hewa yana maana hatuwezi tena kutegemea mazao asili na mavuno pekee kama ilivyokuwa zamani. |
| **30. LORNA:** | Je hii inasababishwa na mikondo ya hali ya hewa inayobadilika? |
| **31. MRS KIMAU:** | Ndio, hali hii inafanana na El Niño-li. Inatishia mifumo yetu ya chakula. Ni tatizo kubwa linalotia hofu! |
| **32. LORNA:** | Kwa hiyo ndio sababu mwakilishi wa Umoja wa Matifa yuko hapa? |
| **33. MRS KIMAU:** | Yaonekana wanahitaji kutafuta mikakati kadhaa kupanda aina tofauti za mimea au hata kuanzisha upandaji wa mazao ambayo hatujazoea kuyala! Hata hivyo, Lorna, nashona sketi yako kwani nadhani utaihitaji leo alasiri kwenye mkutano na waandishi wa habari. |

**35. LORNA:** Asante Mama! Nina wasiwasi kuhusu mkutano huo - juhudi zetu zote za miezi michache iliyopita na halafu tusikie matokeo  katika televisheni ya taifa!

**36. MRS KIMAU:** Hiyo ndiyo karne ya 21 kwako. Haya, hii hapa sketi yako iko tayari.

## Scene Three: Press conference

**37a ALL:** **Chatter**

**37b. ALEX:** Siamini kwamba wanachama wa bodi ya taifa ya umeme wangeweza kuketi chini na kuzungumza nasi ana kwa ana.

**38. JOSHUA:** Ni kweli Alex!  Iliwabidi wachapishe habari za uongo kukanusha taarifa yetu. Inaudhi!

**39. MRS KIMASI:** Lakini Joshua, kumbuka hii haituhusu sisi na kutaka kuonekana kwenye vyombo vya habari! Inahusu mabadiliko ya hali ya hewa na endapo wataacha kujenga kiwanda hiki cha umeme na kutafuta nishati inayoweza kutumia tena, kila mtu atashinda!

**40. CAROL:** Kweli kabisa! Ni wazo zuri. Oh hebu watazame wanakuja humu chumbani.

**SFX:** **CLICKING OF CAMERAS**

**41. MR KAPOOR:** Habari za mchana nyote na waandishi wa habari! Sisi katika bodi ya taifa ya umeme, tunafanya kazi kuwapa umeme na nishati wananchi. Hilo ndilo lengo letu, na siku hizi hilo ni muhimu zaidi kutuwezesha kuendelea kama taifa.

| | |
|---|---|
| **42. JOURNALIST 1:** | Bw Kapoor, je utaendelea na ujenzi wa kiwanda hiki kinachotumia mafuta ya dieseli ingawa athari zake kwa mabadiliko ya hali ya hewa huenda zikawa kubwa? |
| **43. MR KAPOOR:** | Kama kampuni ya ubunifu na inayofikiria siku za usoni, tunaendelea na mipango yetu ya ujenzi wa kiwanda hiki, lakini tutatumia nishati inayoweza kutumika tena na tena na isiyochafua mazingira! |
| **SFX:** | **MURMURS OF SURPRISE** |
| **44. JOURNALIST 2:** | Ni aina gani ya nishati unayozungumzia? |
| **45. MR KAPOOR:** | Tunashirikiana na wawekezaji wa hapa nchini na mataifa ya kigeni, kujenga kiwanda kitakachozalisha umeme kutumia maji. Umeme huu ni mojawapo ya vyanzo safi kabisa vya nishati na pia ni gharama yake ni nafuu na ya kutegemewa zaidi. |

**46. JOURNALIST 2:** Kiwanda hicho kitajengwa wapi?

**47. MR KAPOOR:** Tayari tumeanza mashauriano na jamii zinazoishi kando kando ya Mto Tana. Hapa ndipo tunapokusudia kujenga bwawa. Itachukua muda mrefu kujenga bwawa hilo kuliko mpango wetu wa awali wa kujenga kiwanda cha umeme unaotokana na mvuke. Lakini tunaamini kuwa kwa minajili ya kupunguza mabadiliko ya hali ya hewa, hili ndilo suluhisho bora zaidi.

**48. JOURNALIST 1:** Na je kuhusu jamii zinazoishi karibu na bwawa hilo? Zitapelekwa sehemu nyingine? Au zitalipwa fidia?

**49. JOURNALIST 2:** Na je vipi kuhusu athari kwenye mazingira karibu na mto Tana? Kwa mfano, kupotea kwa maeneo ya wanyama kuishi. Mumefikiria kuhusu athari hizi?

| | |
|---|---|
| **50. MR KAPOOR:** | Sitaki maswali zaidi sasa! Masuala haya yote yanashughulikiwa, lakini jambo muhimu zaidi ni kwamba wakaazi wa mji wa Dhowville watapata umeme hivi karibuni. Na zaidi, umeme safi unaoweza kutumiwa tena na tena. Asanteni sana! |
| **SFX:** | **CLICKING CAMERAS** |
| **51. MR KAPOOR:** | Asante, ni hayo tu! |
| **52. MRS KIMASI:** | Mmesikia wenyewe. Mmefanya kazio nzuri sana! Hatimaye bodi ya taifa ya umeme imeona umuhimu huo na kubatilisha msimamo wao! |
| **53. LORNA:** | Lakini bado siamini, nahisi kana kwamba naota! |
| **54. CAROL:** | Ndio, hata mimi pia nahisi hivyo! Tumefanikiwa kusimamisha ujenzi wa kiwanda hiki! Lakini waandishi wa habari walibuni sababu kupinga ujenzi wa kiwanda cha nishti inayoweza kutumika tena na tena. |

**55. MRS KIMASI:** Kila jambo halikosi kasoro. Hakuna suluhisho lisilo na ila. Tumegundua suluhisho lenye athari chache. Labda ningeweza kuwasiliana nao kuona ikiwa kuna uwezekano wa kujenga matabo ya upepo. Halafu pengine bwawa hilo la umeme unaotokana na maji halitakuwa kubwa kiasi cha kuathiri mazingira na wenyeji wa eneo hilo. Lingekuwa jambo bora kama tungeunganisha umeme unaotakana na maji na upepo. Lakini tukumbe kilicho muhimu. Tumeshinda! Mji wa Dhowville pia utaingia katika historia kama mji wa kwanza kabisa kutumia nishati inayozingatia usafi wa mazingira na inayoweza kutumika tena na tena. Na kama hilo si jambo la kufurahia na kusherehekea, Lorna, basi sijui tufanye nini.

| | |
|---|---|
| **56. ALEX:** | Ni kweli kabisa, nadhani tunahitaji usiku wa mapumziko! Tusherehekee sasa jamani! |
| **57. JOSHUA:** | Nafikiri katika siku zijazo, watu watatushukuru kwa juhudi zetu. Lakini sidhani kazi yetu imekwisha. Naamini bado kuna mengi tunayoweza kufanya kupunguza kasi ya mabadiliko ya hali ya hewa. Niko tayari kwa changamoto hiyo! Usijali bwana sisi ndio kikosi maalum! Hakuna kitu kitakachotuzuia sasa! |
| **58: ALL:** | Ndiyo! Kweli tumefaulu! |

**END OF EPISODE 10**

**Outro:**

Na hadi hapo msikilizaji tunafika mwisho wa kipindi hiki cha kumi na cha mwisho kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa. Mchezo huu umeandikwa na Victoria Averill. Kumbuka ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki tembelea tovuti yetu www.dw-world.de/lbe Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa na asante kwa kusikiliza!